JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI ISIMILA

Namba za Simu
Mkuu wa Shule: 0753080790
Makamu Mkuu wa Shule: 0755633093
Matron: 0767167954

S.L.P. 1459,
IRINGA.

30/3/2022

MZAZI WA .....
S.L.P..... .....

YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA ISIMILA SEKONDARI HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA, MKOA IRINGA 2022/2023</u>

Nafurahi kukupongeza kwa kufanikiwa kufaulu na kukuwezesha kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ISIMILA kuanza cha tano, **hongera sana**.

Ni matumaini yangu kuwa utatumia vizuri nafasi hii na kwamba utatumia **JUHUDI** na **MAARIFA** ya hali ya juu ili uweze kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, usafi na michezo.

Shule ya Sekondari Isimila ni shule ya bweni. Shule ipo umbali wa Km 26 kutoka Iringa Mjini na Km 10 kutoka barabara kuu iendayo Mbeya upande wa Mashariki (Sehemu iitwayo Wenda au Njiapanda ya Mlolo). Shule itafunguliwa tarehe ..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

Kwa wanafunzi watakaofika siku tatu (03) za mwanzo watasafirishwa na gari la shule kutoka Wenda mpaka shuleni. Mabasi yanapatikana stendi kuu Iringa kwa nauli ya shilingi 2,500/=

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Isimila Sekondari.

.....
FRANK MAHENGE
MKUU WA SHULE
ISIMILA SEKONDARI

ADA NA MICHANGO

ADA YA SHULE

Ada ya shule ni Tsh. 70,000/= kwa mwaka, kwa muhula ni Tsh. 35,000/= na ziingizwe kwenye akaunti ya shule Na. **60501100065 NMB** Jina la akaunti **ISIMILA SEKONDARI**. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye BPS)

MICHANGO MINGINE NA VIFAA VYA KULETA SHULENI

1.	Tsh. 5,000/=	Kwa ajili ya tahadhari/Kinga (hazirudishwi)
2.	Tsh. 10,000/=	Kwa ajili ya matibabu
3.	Tsh. 6,000/=	Kwa ajili ya kitambulisho na picha
4.	Tsh. 30,000/=	Kwa ajili ya kuchangia ulinzi, wapishi, vibarua wengine
5.	Tsh. 20,000/=	Kwa ajili ya kuchangia taaluma
6.	Tsh. 15,000/=	Kwa ajili ya ukarabati wa samani
7.	Rimu moja ya karatasi A4	Hatupokei fedha
8.	Ndoo 2 za ujazo wa lita 10	
9.	Fagio ngumu na jembe	
10.	Tsh. 2,000/=	Kwa ajili ya nembo ya shule
11.	Tsh. 5,000/=	Kununua umeme wa shule
12.	Tsh .5,000/=	Marekebisho ya gari ya shule
13.	Tsh. 4,000/=	Kuweka nembo kwenye T -Shirt

Fedha hizi ziingizwe kwenye akaunti namba **60501100065 NMB** jina la akaunti **ISIMILA SEKONDARI** na stakabadhi za benki kuletwa shuleni. **Hatupokei fedha taslimu**.

- Godoro la futi 2.5” x 6”
- Shula mbili rangi ya bluu bahari
- Blanketi
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli na kikombe vya mfupa) na kijiko
- Daftari za kutosha (counter books)
- Ingawa shule ina vitabu unashauriwa kuja na vitabu vya kujisomea kulingana na masomo yake (orodha imeambatanishwa)
- Scientific calculator

SARE ZA SHULE

1. Blauzi mbili (2) tetroni nyeupe mikono mifupi
2. Sketi 2 (marinda madogo ya kawaida) rangi ya sketi
3. Jozi mbili za viatu vyeusi visivyo na kisigino kirefu vya shuleni vya kufunga na kamba
4. Jozi mbili za soksi nyeupe
5. Sweta ya rangi ya bluu yenye shingi "V" isiyopasuliwa mbele
6. Tsh. 10,000/= kwa ajili ya T-shirt ya shule
7. Raba jozi moja na nguo za michezo yaanu bukta, sketi, tracksuit (blue bahari)
8. Nguo za kazi (shamba dress) rangi ya bluu bahari (light blue) gauni solo.
9. Kanga doti mbili
10. Taulo
11. Rimu moja (1) ya A4

Kwa waislamu

12. Mtandio mweupe (hijabu ndefu) isiyo na urembo
13. Nusu kanzu isiyobana ya rangi nyeupe mikono mirefu

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo ambazo siyo sare ya shule. Ukaguzi utafanyika mwanafunzi anaporipoti shuleni.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

(a) WAKUBWA WANAOKUZIDI

(i) Kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo

(ii) Kutumia lugha nzuri wakati wote.

(iii) Kushirikiana na kusaidiana na mwanafunzi wengine katika kazi.

(iv) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

(v) Kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mkuu anayekuita

(vi) Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa vyama na serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.

(vii) Kukaa kimya darasani na kutoka kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko darasani.

(viii) Mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na nje ya shule.

(b) BAADHI YA TABIA ZISIZORUHUSIWA KWA WANAFUNZI

(i) Kuvuta sigara, kutumia dawa za kulevya, pombe n.k

(ii) Kufuga kucha ndefu, ndevu au nywele ndefu/chafu

(iii) Kuvaa mavazi yasiyokubalika au yasiyo ya heshima

(iv) Uasherati, wizi, utapeli n.k.

(c) SARE

- Unapaswa kuwa na sare za shule kwa mshono uliokubalika na kwa wakati kama unapopangiwa

(a) Wakati wa amsomo darasani

(b) Safari zote za nje ya shule kwa jina la shule

(c) Unapotoka au kwenda likizo

- Unapaswa kuwa na nguo za michezo na vazi la kazi za mikono kama itakavyoelekezwa (shamba dress)

MIPAKA YA SHULE

(i) Unapaswa kufahamu mipaka ya shule na kuto kutoka nje ya mipaka hiyo.

(ii) Pasi maalumu ya kutolea ruhusa itatolewa na mwalimu wa zamu au mwalimu wa malezi na itaidhinishwa na Mkuu wa shule kila inapokwenda nje ya shule.

(iii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea maeneo yafuatayo:-

1. Ofisi ya walimu
2. Ofisi ya Mkuu wa Shule
3. Nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa maalum.
4. Hairuhusiwi kabisa kwa wanafunzi kutembelea
   (a) Vilabu vya pombe
   (b) Majumba ya starehe
   (c) Nyumba za kufikia wageni (Guest House)

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Ulezi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xiii) Kutembelea nyumba za walimu, Ofisi ya Mkuu wa shule pamoja na ofisi ya walimu bila ruhusa au sababu ya msingi.

(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xv) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa simu n.k.

(xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu ya maisha yake ya kila siku, hivyo mwanafunzi atahusika na:-

(a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi

(b) Usafi wa maeneo (viwanja vya shule)

(c) Usafi wa madarasa na bweni analoishi

MATUMIZI NA UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE NA MAZINGIRA

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza vizuri mali za shule kama vile majengo, viti, meza, madawati, ndoo, vitabu, vifaa vya madarasani n.k.

(b) Weka mazingira ya shule katika hali ya usafi na ya kuvutia. Okota karatasi au uchafu wowote, pita kwenye njia za miguu, usikatishe ovyo na kukanyaga majani au maua.

8.0 **UTORO**

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shule bila taarifa atahesabiwa ni mtoro. Taarifa kuhusu mwanafunzi asiyehushuria kutokana na matatizo yoyote lazima ziwasilishwe shuleni siku hiyo ya matatizo kwa mwalimu wa zamu au mwalimu wa malezi au Mkuu wa shule na mzazi au mlezi anayetambuliwa na shule kulingana na fomu ya usajili.

ORODHA YA VITABU

1. KISWAHILI

1.	NADHARIA YA LUGHA	MASEBO, J.
2.	KISWAHILI KIDATO CHA 5 &6	OXFORD UNIVERSITY PRESS
3.	NADHARIA YA FASIHI	MASEBO, J.
4.	TAHAKIKI	

2. ENGLISH LANGUAGE

1.	ADVANCED ENGLISH LANGUAGE	OXFORD
2.	ENGLISH LANGUAGE	NICHOLAUS ASHEL
3.	LITERATURE IN ENGLISH	

3. GEOGRAPHY

1.	PHYSICAL GEOGRAPHY	MSABILA
2.	HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY	MSABILA
3.	PHYSICAL GEOGRAPHY	MONK HOUSE
4.	PHYSICAL GEOGRAPHY	BUNNET
5.	INTERGRATED GEOGRAPHY	DAVID WAUGH

4. HISTORY

1.	ADVANCED LEARNER'S HISTORY 5 & 6	OXFORD
2.	MASTERIAL HISTORY	CARTER
3.	HISTORY FOR ADVANCED	ZISTI KAMILE

5. ECONOMICS

1.	ECONOMICS ADVAANCED LEVEL	
	PAPER 1	C.M. AMBILIKILE
	PAPER 2	C.M AMBILIKILE

KISWAHILI

- FUNGATE YA UHURU
- KIVULI KINAISHI

- CHUNGU TAMU
- KWENYE UKINGO WA THIM
- NGUZO MAMA
- MFADHILI
- MORANI
- KIMBUNGA
- MAPENZI BORA
- USIKU UTAKAPOKWISHA

ENGLISH LANGUAGE

- RWANDA MAGERE
- HIS EXCELLENCE THE HEAD OF STATE
- I WILL MARY WHEN I WANT
- BETRAYAL IN THE CITY
- THE BRIDE
- DEVINE PROVINCE
- A MAN OF THE PEOPLE
- THE BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI ISIMILA

S.L.P. 1459,
IRINGA.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ISIMILA
S.L.P 1459,
IRINGA.

MWANAFUNZI

Mimi ..... nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako na sheria zake. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nakubali/sikubali nafasi hiyo kwa sababu ..... pia nayakubali/siyakubali masharti/sheria za shule yako.

A: MZAZI/MLEZI

Mimi ..... Mzazi/Mlezi wa ..... Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako, nimesoma maagizo ya kujiunga na shule pia sheria zake. Ninakubali/sikubali nafasi hiyo (**kwa anayekubali**). Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule hiyo katika muda uliopangwa. Pia nitashirikiana daima na shule yako katika kumkuza na kumlea mtoto wangu.

B: AHSANTE

Jina la Mzazi/Mlezi .....

Anuani yake .....

Mtaa/Kitongoji anapoishi .....

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
ISIMILA SECONDARY SCHOOL
P.O Box 1459
IRINGA – TANZANIA

TO BE COMPLETED BY Medical Officer in respect of all form I entrant

1. Full name ……
2. Age …… Year …… Sex ……..
3. Blood Count (Red and White) ……..
4. Stool examination ……
5. Urine analysis ……
6. Syphilis test ……
7. Eye test ……
8. TB test ……..
9. Ears ……..
10. Chest ……..
11. Spleen ……
12. Abdomen ……..

ADDITIONAL INFORMATION: Eg. Physical Disability (If any)

……

……

……

I certify that the above named student is fit to pursue studies

Signature ……. Designation ……..

Section …….. Date ……..

Official stamp ……..

STUDENT

You must bring this complete when you come to school. No student may be enrolled without certificate of physical fitness.